JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI TALLO,
S.L.P 99
NGUDU -KWIMBA.

Tarehe…………………………

NAMBA ZA SIMU:
MKUU WA SHULE: 0788 221 885
MAKAMU MKUU WA SHULE: 0686 513 129
MWALIMU WA TAALUMA: 0765 033 388

Jina la Mwanafunzi………………………………………
S.L.P………………………………

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TALLO ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA MKOA WA MWANZA KIDATO CHA TANO MWAKA……………………..

## 1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano (5) katika shule hii mwaka………….tahasusi ya ....................HONGERA SANA. Unatakiwa kuripoti hapa shuleni tarehe……………….bila kuchelewa kabla ya saa 11:00 jioni na mwisho wa kuripoti ni baada ya wiki mbili tangu shule ifunguliwe. Mwanafunzi atakaye chelewa zaidi ya wiki mbili atakuwa amepoteza nafasi yake. Shule hii ina tahasusi zifuatazo: EGM, HGK na HGFa.

Mwanafunzi ajaziwe Fomu ya vipimo vya afya na Fomu ya maelekezo juu ya mwanafunzi. Fomu hizi zimeambatishwa kwenye barua hii. Hakikisha zimejazwa kikamilifu kwa mujibu wa maelekezo kisha uje nazo siku ya kuripoti.

## 2.0 MAHALI SHULE ILIPO.

Shule ya Sekondari Tallo inapatikana Wilaya ya Kwimba, Mkoa wa Mwanza umbali wa Kilomita 78 kutoka Mwanza Mjini. Endapo utatumia usafiri wa MABASI shuka kituo cha mabasi Nyegezi au popote pale mtakapo shushwa ndani ya Jiji la mwanza, panda daladala elekea Stendi ya mabasi ya NYAMHONG’ORO, hapo kuna Coaster na Basi za kwenda Nyambiti -KWIMBA ilipo Shule ya Sekondari Tallo. Njia ya pili panda kuelekea Kisesa Stendi mpya utakuta haisi za kwenda Nyambiti - Kwimba, ukifika Nyambiti uliza

Tallo Sekondari utakuwa umefika au fika Wilaya ya Magu Mjini panda Haisi za Magu-Nyambiti- Ngudu shuka NYAMBITI Senta au NKALALO Senta na uliza TALLO Sekondari.

3.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

3.1 SARE YA SHULE

▪ Shati nyeupe aina ya tomato pamba yenye mikono mirefu jozi (2) isiyobana mwili au kupenyeza mwanga na iwekewe alama ya “V” yenye rangi nyeusi kwenye bega la mkono wa kushoto ikiwa na maana ya kidato cha tano. Shati za kushona haziruhusiwi wala kitambaa cha arua hakiruhusiwi kuvaliwa hapa Shuleni.

▪ Suruali nyeusi yenye Malinda manne mbele isiyobana, nyuma iwe na mfuko mmoja pia iwe na tanapu, isiwe modo au pisto. Chini iwe nchi 16 kitambaa kizito cha suti jozi 2. Suruali isiyo kidhi masharti ya hapo juu, haitapokelewa. Kitambaa kiwe ISITIMU GRADE ONE isiyopauka haraka.

▪ Tisheti rangi ya KIJANI yenye kola jozi moja (1). (iweza patikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 12,000/= kwa mzazi atayehitaji).

▪ Sweta (1) moja rangi ya dark blue iliyo na rangi moja na yenye mkato wa alama V.

▪ Viatu vya rangi nyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba jozi mbili (2), KUMBUKA Mabuti na viatu vya shingo ndefu havikubariki

▪ Soksi rangi nyeusi jozi mbili (2) au zaidi isiyo na maandishi yoyote.

▪ Mkanda mweusi wa Suruali usio na chuma kikubwa wala maandishi yeyote.

▪ Tai moja Nyeusi au zaidi yenye mistari ya pundamlia yenye nembo ya shule (inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh 5,000/= kwa mzazi atakayehitaji).

▪ Blanket moja (1) kwa ajili ya baridi.

3. 2 SHAMBA DRESS (NGUO ZA KUSHINDIA)

Suruali mbili rangi ya khaki isiwe modo, chini iwe inchi 16 iwe na tanapu, mfuko mmoja Nyuma.

Tisheti mbili (2) rangi ya Machungwa (Orange) (unaweza kuzipata shuleni kwa gharama ya sh 12,000/=kwa mzazi atakayehitaji.

Nguo za michezo:

(i) (Bukta ya rangi nyeusi na tisheti ya rangi nyeusi zenye michirizi mieupe.

(ii) Track-suit rangi ya KIJIVU kwa ajili ya michezo na muda wa baridi.

Raba za michezo (rangi yoyote).

N.B:Kwa wale watakaopenda kushonewa /Kuandaliwa sare za Shule katika mazingira ya Shule, zinaweza kupatikana kwa gharama zifuatazo:

| | |
|---|---|
| Shuka mbili (2) za rangi ya kijani @ Tsh.10,000/= | 20,000/= |
| Suruali mbili (2) za darasani rangi nyeusi @ Tsh.20,000/= | 40,000/= |
| Suruali mbili (2) za kushindia rangi ya khaki @ Tsh.20,000/= | 40,000/= |
| Tshirt moja (1) ya darasani rangi ya kijani yenye nembo ya shule Tsh.12,000/= | 12,000/= |
| Tshirt mbili (2) Za kushindia rangi ya machungwa yenye nembo ya shule @ Tsh.12,000/ | 24,000/= |
| Jezi ya michezo bukta na tshirt yake rangi nyeusi | 10,000/= |
| Godoro 2.5"x6" | 45,000/= |
| Chandarua rangi Nyeupe | 10,000/= |
| JUMLA | 201,000/= |

Fedha hizi zilipwe Tsh. 201,000/=Cash Ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule

Jukumu la matibabu ni la mzazi/mlezi, unatakiwa kumlipia mwanao BIMA ya Afya ya Taifa (NHIF), hivyo mtoto aje na KADI ya Bima ya afya ya NHIF na kwa mwanafunzi ambaye hana KADI YA BIMA ya afya ya NHIF aje na Tsh 50,400/=. Fedha hii ikabidhiwe TASLIMU Ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule siku ya kulipoti shuleni bila kukosa kwa sababu matibabu ni gharama za mzazi/mlezi siyo Shule.PESA YA BIMA ISILIPWE BENKI.

NB: Mahitaji yake binafsi kama vile Daftari, sabuni, dawa ya meno, kitana, mswaki, mafuta ya kupaka, brashi, saa ya mkononi, peni, penseli, rula, taulo, saa ya mkononi n.k (vinapatikana kwenye duka la shule). Sanduku la bati (tranka) aje nalo.

TANIBIHI: Mwanafunzi aje amevaa mojawapo ya sare za shule tajwa hapo juu. Aidha nguo za nyumbani haziruhusiwi kuingia wala kuvaliwa shuleni au eneo la shule kwa muda wote utakaokuwa Shuleni.

4. VIFAA VYA USAFI

Mfagio moja (1) ngumu (Hard bloom) (HGK, HGFa).

Mfagio moja (1) laini wa ndani (Soft bloom) (EGM).

Mfagio mmoja (1) wa nje (chelewa) wenye mpini uliofungwa kwa waya (EGM, HGK, HGFa).

Jembe moja (1) na mpini wake (EGM, HGK, HGFa)

Mopper (1) (mfagio wenye mpira/laba) kwa ajili ya kusukumia maji (HGK, HGFa).

Lita tano (5) ya dawa ya kufanyia usafi wa vyooni (EGM, HGK, HGFa).

Brush/mfagio mgumu moja (1) wa kusafishia vyooni (EGM).

Tafadhali leta vifaa KAMWE usilete pesa shuleni haitapokelewa.

5. MICHANGO MUHIMU YA SHULE

| Na. | Aina ya michango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

Shule haipokei Fedha taslimu, zilizoainishwa kwenye kipengele namba 5 hapo juu"Fedha zote zilipwe kupitia Akaunti ya Shule katika Benki ya NMB namba ya akaunti ni 3150 1100 463 Jina la akaunti ni TALLO SECONDARY SCHOOL (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip). Mwanafunzi alete pay in slip halisi ya Benki na sio kivuli cha pay in slip.

6. MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANATAKIWA KULETA SHULENI NI:

i. Mabunda mawili (2) ya Karatasi (Ream (2) aina ya Double A) kwa Mwaka, aina nyingine za ream hazitapokelewa. (ATAKABIDHI).
ii. Vitabu vya masomo vya tahasusi husika angalau viwili kwa kila somo.
iii. Kitabu kimoja kwa kila aina ya vitabu teule vya Kiswahili na Fasihi ya Kiswahili (Riwaya, Tamthiliya na Ushairi) (orodha imeambatishwa kwa wanafunzi wa HGK na HGFa.
iv. (Aje na Godoro moja size 2.5"x 6" la sponji (inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh 45,000/= kwa mzazi atakayehitaji).
v. Madaftari makubwa (Counter Book) walau Kumi (10) au zaidi Quire 3 au 4 kwa matumizi ya darasani.
vi. Mashuka mawili (2) rangi ya KIJANI.
vii. Chandarua kimoja saizi maalum (Rangi nyeupe).
viii. Ndoo 3, mbili ya lita 20 kwa ajili ya kutunzia maji yanapokatika na moja ndogo ya lita 10 ya kuogea zenye mifuniko, galoni moja la lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa.
ix. Begi dogo la kubebea daftari na vitabu. Ni marufuku kubeba daftari kwa kutumia gazeti au mikononi.
x. (x) Kikokotozi (Scientific Calculator) kwa wanafunzi wa TAHASUSI YA EGM. Unaweza kuinunua shuleni kwakiasi cha Tsh.50, 000/=.

xi. (xi) Vyombo vya chakula kama vile sahani, kontena (bakuli lenye mfuniko), kikombe na kijiko, (xii) Mto wa kulalia pamoja na foronya yake rangi ya shuka.

xii. (xiii) Spring file kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi. (xiv) Kanzu moja nyeupe kwa wanafunzi wa kiislam.

xiii. Rimu moja (1) ya RULLED PAPER (karatasi zenye misitari) kwa ajili ya mazoezi darasani. ATAITUNZA MWANAFUNZI MWENYEWE.

xiv. Kalamu za wino na penseli za kutosha.

xv. Mkebe wa Hisabati kwa wanafunzi wa tahasusi zote.

xvi. Taa yakuchaji kwa jua ama taa ya betri kwa tahadhali ya umeme ukikatika (isiwe ya kuchaji kwa umeme.

Kandambili za kuogea.

## 7. SHERIA ZA SHULE

### A. HESHIMA.

Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:

i. Anatakiwa kusimama na kusalimia mwalimu, mfanyakazi na mtu yeyote anayemzidi umri.

ii. Anatakiwa kuheshimu wafanyakazi wote, wanafunzi wenzake na jamii yote anayoweza kukumbana nayo.

iii. Anapaswa kuthamini, kuheshimu na kutekeleza kazi zote anazopewa ndani na nje ya darasa.

iv. Anatakiwa kuvaa mavazi ya heshima wakati wote.

v. Kuheshimu ratiba nzima ya shule.

vi. Ni marufuku mwanafunzi kujipikilisha au kupeleka chakula bwenini bila ruhusa ya mwalimu.

vii. Anatakiwa kutii amri au wito wa viongozi au walezi wake wakati wote na mahali popote.

viii. Anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, Picha za viongozi, Nembo ya Taifa, Wimbo wa taifa na Fedha ya Taifa.

ix. Haruhusiwi kuingia katika nyumba za wafanyakazi/walimu, ofisi za walimu, maktaba na maabara n.k bila ruhusa.

x. Ni marufuku kupiga makelele mabwenini na madarasani wakati wote awapo shuleni.

xi. Anatakiwa kuheshimu na kukubali tofauti za kidini na kiutamaduni zilizopo katika jamii.

xii. Ni marufuku kushiriki au kuendekeza imani za kishirikina.

xiii. Ni marufuku mwanafunzi kutumia lugha chafu, kugombana mahali popote na kwa mtu yeyote.

xiv. Anatakiwa kuheshimu na kuitika wito toka kwa walezi/walimu pamoja na viongozi wake (viranja), hii ikiwa ni pamoja na mwitiko wa kengele wakati wote anapohitajika.

xv. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki simu hapa shuleni. Akikamatwa na simu awapo shuleni, atafukuzwa shule.

NB: Shule inatoa huduma ya mawasiliano yaliyo rasmi, ya lazima na yenye umuhimu tu. "Ni marukufu kwa mwanafunzi kuvuta sigara, kufuga kucha, kuwa na nywele ndefu, kunyoa kipara, kunyoa mtindo, (mf. Panki,kiduku) na kamwe asiweke dawa.

B. MAHUDHURIO

i. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwahi popote anapotakiwa na kuhudhuria vipindi vyote vya masomo darasani na nje ya darasa ikiwa ni pamoja na "morning parade", "evening roll call" "afternoon prep, "evening prep", "emergence calls", n.k.

ii. Kila mwanafunzi anatakiwa kutoa taarifa ya kutohudhuria shule au kipindi chochote ndani na nje ya darasa kwa mwalimu wa darasa/ mwl. Wa zamu na siyo kiongozi wa darasa yaani (monita).

iii. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano ya mabweni na madarasa.

C. UVAAJI WA SARE

(i) Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule ya darasani muda wote awapo darasani, anapokwenda kanisani au misikitini, kwenda hospitali, na sare ya nje wakati wa shughuli mbalimbali za shule. Ni marufuku kuchanganya sare.

(ii) Ni lazima mwanafunzi avae sare iliyo safi na nadhifu muda wote awapo shuleni au nje ya shule.

ANGALIZO

- Mwanao atavaa sare ya shule kwa kipindi chote atakapokuwa hapa shuleni na hataruhusiwa kuvaa nguo za nyumbani, hivyo hairuhusiwi kuja na mzigo mkubwa wa nguo ambazo hatapata nafasi ya kuzivaa awapo shuleni.
- Vipodozi, pafyum, radio, kamera, simu ya mkononi,laini ya simu,flashi au memory card pamoja na nguo za nyumbani haviruhusiwi shuleni. Ukaguzi utafanyika kabla ya kuingia bwenini na pia unafanyika kwa kushitukiza. Akipatikana navyo, hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule. ZINGATIA.
- Hakikisha mwanao ajapo shuleni, awe amepimwa afya na kujaza fomu ya afya kikamilifu. Hii itatusaidia kuwatambua wanafunzi wenye mahitaji maalumu kimalezi. Aidha, kutakuwa na upimaji afya wa dharura wanafunzi wawapo shuleni
- Kwa wale watakaoshonewa sare zao hapa shuleni watatakiwa kuja wamevaa track suit wakati wanasubiri kushonewa sare za shule.

D. MIPAKA YA SHULE

Mwanafunzi asitoke nje ya mipaka ya shule bila kibali maalumu kwa muda wote anaotakiwa kuwepo shuleni. Ni marufuku mwanafunzi kutembelea salon wakati wote wa vipindi. Ni marufuku mwanafunzi kutembelea nyumba za kulala wageni (Guest houses), vilabu vya pombe (Bar) au majumba ya starehe (Recreation houses). Mwanafunzi haruhusiwi kuingia ofisi ya walimu (Staff room) bila kibali maalumu.

E. USAFI.

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi yeye mwenyewe na kutunza mazingira ya shule, hivyo anatakiwa kuleta vifaa vya usafi: jembe na mpini wake, mfagio mmoja wa kuti (chelewa).

F. KUTEMBELEWA NA NDUGU (VISITING DAY)

Wanafunzi wa bweni wataruhusiwa kutembelewa mara moja tu kwa mwezi na siku hiyo ita kuwa ni Jumapili moja ya kila mwisho wa mwezi. Kwa mwanafunzi atakayekiuka utaratibu wa shule ATAWAJIBISHWA. Daima mwanafunzi atumie muda wake vizuri kitaaluma awapo shule.

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi
ii. ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/
utoro iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla.
iv. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
v. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
vi. Uvutaji wa sigara
vii. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
viii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
ix. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
x. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xi. Kudharau Bendera ya Taifa,Wimbo wa taifa na nyimbo zote za uzalendo.
xii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xiii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

4. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

d) Orodha ya vitabu teule vya Kiswahili na Fasihi ya Kiswahili

e) Orodha ya vitabu vya tahasusi vya mtaala mpya.

f) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

ZINGATIA, Shule ina program na taratibu zake zenye kulenga kuinua na kuendeleza Taaluma shuleni. Mwanafunzi ni LAZIMA azifuate na kuzitekeleza. Hizi ni pamoja na kutumia lugha ya Kiingereza katika mawasiliano yote muda wote awapo shuleni. Kuhudhuria prepo wakati wa jioni na hata usiku kwa mujibu wa ratiba. Pia kuhudhuria mihadhara mbalimbali ya masomo, yaani “DEBATES” na “SUBJECT CLUBS”. Hii sio hiari ni LAZIMA.

5. TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

KARIBUNI SANA!!!

........................

SAMWEL J. MAILA
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI TALLO
S.L.P. 99
NGUDU-KWIMBA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI TALLO,

S. L. P 99,

NGUDU – KWIMBA.

FOMU YA KUKIRI KWA MZAZI/MLEZI KUKUBALIANA NA SHERIA, TARATIBU, KANUNI NA MAELEKEZO MBALIMBALI YA SHULE JUU YA MWANAFUNZI.

Mimi ………………………………………………… ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ……………………………………………………. Nakiri kuwa nimezisoma mbele yake na kuzielewa vyema sheria, taratibu, kanuni na maelekezo mbalimbali atakayopewa mtoto wangu hapa shuleni.

Nimekubaliana nazo na endapo atafanya kunyume sitamtetea, badala yake nitakubaliana na kuheshimu maamuzi yatakayotolewa na Uongozi wa Shule au walezi wake.

Jina la mzazi/mlezi…………………………………………………

Saini………………………………

Tarehe ……………………………

Jina la mwanafunzi……………………………….. Saini ……………
Tarehe ……………

KWIMBA DISTRICT COUNCIL

# TALLO SECONDARY SCHOOL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

FROM: THE HEADMASTER,
TALLO SEC.SCHOOL,
P.O.BOX 99,
NGUDU/KWIMBA.

Please examine the student, (named)…………………………………………………. To his physical and mental fitness for a full time student.

## MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the following student named above and consider his fitness for re – engagement as above: this is certified by the following results of my examination:

1. Bilharzias …………………………………
2. Jaundice……………………………………
3. Scabies…………………………………….
4. Typhoid…………………………………….
5. Abdomen…………………………..……
6. Tropical ulcer………………………………
7. Hemoglobin…………………..…………
8. Abscesses…………………..…………..
9. Asthma……………………………………..
10. Leprosy…………………………………….
11. Small pox…………………………………..
12. Heart failure………………………………..
13. Cystitis……………………………………..
14. Diabetes……………………………………..
15. Epilepsy……………………………………..
16. STDs…………………………………………
17. Headache……………………………………..
18. Osteomyelitis…………………………..…
19. Bronchopneumonia…………………………
20. Skin disease…………………………………
21. TB……………………………………………

OTHER EXAMINATIONS

1. Eyes………………………….
2. Chest………………………….
3. Any abnormalities noted……….
4. Any chronic complaints not noted ………………………………….

NOTE: in case of TB and Bilharzias it is recommended that a student should attend a clinic/medical treatment before he come to school.
Name and signature of Medical officer / Examiner…………………………………… Designation and official Stamp …………………………………………………,……..
Date ……………………………

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

FOMU YA URAIA

1. Jina la mwanafunzi……………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa …………… mwezi …………… Mwaka……….
3. Jina la Baba ………………………………………………………………………..
4. Mahali alipozaliwa:
   (a) Kijiji/ mtaa ………………………………..
   (b) Wilaya ……………………………………..
   (c) Mkoa ………………………………………
5. Ni raia wa Tanzania …………………………………………………
6. Nambari na tarehe ya Hati ya Uraia iwapo si kwa kuzaliwa:

   ……………………………………

7. Si raia wa Tanzania ni raia wa ……………………………………………………..…….
8.Jina la Mama ……………………………………………………………………………
9. Mahali alipozaliwa:
   (a) Kijiji/ mtaa ……………………………………………………….....
   (b) Wilaya ………………………………………………………….....
   (c) Mkoa ………………………………………………..…………
10. Ni raia wa Tanzania

    ……………………………………………………………………………………………

11. Nambari na tarehe ya Hati ya Uraia iwapo si kwa kuzaliwa:

    ……………………………………………………………………………………

12. Si raia wa Tanzania ni raia wa …………………………………………….

    Saini ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa au saini ya Afisa Mtendaji wa Kata

    ……………………………

    Muhuri ……………………………………….. Tarehe …………………………………….

OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI TALLO

FOMU YA MAELEZO JUU YA MWANAFUNZI

| MATUMIZI YA OFISI TU |
|---|
| NA. YA USAJILI : |
| TAREHE YA KURIPOTI : |

1. Jina kamili …………………………………………………. (ulilotumia katika shule uliyotoka).
2. Dini yako/Dhehebu ……………...…………..
3. Tarehe ya kuzaliwa....... Mwezi…… Mwaka……..Wilaya……………Mkoa……………
4. Shule uliyotoka …………………………… Wilaya ………..…... Mkoa…..…………
5. Michezo uipendayo au shughuli (hobbies) uzipendazo:

   ……………………………………………………………………………………………..
6. Ulemavu au historia ya ugonjwa (Tafadhali taja)…………………
7. Unaishi na nani, mzazi au mlezi?........................ Taja jina lake,…………………………

   Kama unaishi na mlezi, taja uhusiano:…………………
8. Kazi ya Mzazi/Mlezi……………………………
9. Mahali anapoishi: Wilaya …………Mkoa……………

   Anwani ……………………………...Simu…………………………

10. Jina na anwani ya mtu atakayetumiwa ripoti yako ya maendeleo ya masomo na mambo mengine:

    Jina lake kamili…………………………….. Uhusiano……………………………..

    Anwani …………………………………….        Simu ………………………………

11. Ndugu wanne (4) watakaokutembelea hapa shuleni na namba zao za simu:

| JINA | UHUSIANO | ANAPOISHI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

12. Jina la mji na kituo cha usafiri (uwanja wa ndege, bandari, stesheni ya reli na kituo cha basi) utakachoshukia wakati wa likizo zako……………………………………………………………...

Tamko la mwanafunzi:
"Nimezisoma na kuzielewa Sheria na Kanuni za Shule, ninaahidi kuzifuata na kuzitekeleza"

Sahihi ya Mwanafunzi ………………………………… Tarehe ………………………………
Sahihi ya Mzazi/Mlezi ………………………………… Tarehe ………………………………

HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

SHULE YA SEKONDARI TALLO

FOMU YA KUANDIKISHWA NA AHADI ZA UTII (Ijazwe Kwa herufi kubwa na irudishwe kwa Mkuu wa Shule)

1. (a) Jina kamili……………………………………………………………….

(b) Tarehe ya kuzaliwa………………………………………………..

Kijiji/kata……………………………Wilaya…………………………………..

Mkoa…………………………….…Taifa………………………………………

(e) Shule unayotoka:……………………………………………………………………….

2. Jina kamili la Baba au mlezi………………………………………………………

Anwani yake………………………………………………………………………..

Kazi ya Baba au mlezi……………………………………………………….

3. AHADI ZA MWANAFUNZI

(a)Mimi……………………………………………………………………………

Nime yasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria za shule.

Na yakubali na niko tayari kuwa mwanafunzi wa TALLO ya sekondari.

Na ahidi kwamba

i. Nitatimiza masharti yote ya shule ii. Nitatii sheria za shule nikikiuka ahadi zangu nitachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Tarehe………………………… Sahihi ya mwanafunzi…………………………………..

AHADI ZA MAZAZI

Mimi……………………(Mzazi au Mlezi)wa Mwanafunzi ……………………………

Nimeelewa maelekezo ya shule kwa mwanafunzi huyu.

Hivyo na naahidi kwamba

(i) Nitashirikiana kikamilifu na uongozi mzima wa shule katika kumwelimisha na Kumlea ipasavyo.

(ii) Nitatimiza masharti yake ya shule

(iii) Sita mkatiza masomo kwa minajiri ya shughuli za familia

(iv) Nitafanya kila jitihada kumwezesha mwanangu kuwahi shule kila siku na kufika Shule ni siku ya kufungua shule bila kuchelewa

Tarehe…………………………… Sahihi ya mzazi/mlezi………………………….

SHULE YA SEKONDARI TALLO

ORODHA YA VITABU KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO 2026/2027

| SOMO | JINA LA KITABU | MWANDISHI |
|---|---|---|
| HISTORY | 1.History for Advanced Secondary School Form Five (New Syllabus).<br>2.History for High School Form Five New Sylabus (2023) | TIE<br>Bakari Madaya |
| GEOGRAPHY | 1.Pysical Geography for Advanced Secondary School Form Five & Six<br>2.Practical Geography for Advanced Secondary School Form Five & Six<br>3. Aje na kitabu cha ziada cha mtaala mpya. | TIE<br>TIE |
| ADVANCED MATHEMATICS | 1.Advanced Mathematics for Secondary School Form Five (New Syllabus). | TIE |
| ECONOMICS | 1.Microeconomics for Advanced Secondary Schools Form Five (New Syllabus).<br>2.Microeconomics Made Simple for Advanced seccondary School (2023)<br>3.Macroeoeconomics Made Simple for Advanced Seccondary School (2023) | TIE<br>Mwakagile,E<br>Mwakagile,E |
| ACADEMIC COMMUNICATION | 1.Academic Commucation for Advanced Secondary School Form Five (New Syllabus). | TIE |
| FASIHI YA KISWAHILI | 1.Kiswahili Shule za Sekondari Fasihi ya Kiswahili Kidato cha tano (Mtaala mpya)<br>2.Kanzi ya Fasihi ya Kiswahili mtaala mpya (2025) | TIE<br>Mwl.Gwivaha,G.J |
| HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI | 1.Historia ya Tanzania na Maadili Shule za Sekondari Kidato cha tano (Mtaala mpya) | TIE |
| KISWAHILI | 1.Kiswahili Shule za Sekondari Kidato cha tano (Mtaala mpya) | TIE |

1. ORODHA YA VITABU TEULE KIDATO CHA TANO NA SITA MTAALA MPYA: KISWAHILI

A:RIWAYA

| NA. | JINA LA KITABU | JINA LA MTUNZI |
|---|---|---|
| 1. | Dunia Uwanja wa Fujo | Euphrace Kezilahabi |
| 2. | Ua la Faraja | W.E.Mkufya |
| 3. | Mirathi ya hatari | C.G.Mung'ong'o |
| 4. | Wasifu wa Siti Binti Saad | Shaaban Robert |

B.TAMTHILIYA

| NA. | JINA LA KITABU | JINA LA MTUNZI |
|---|---|---|
| 1. | Mukwava wa Uhehe | M.M.Mulokozi |
| 2. | Shujaa Mirambo | Emmanuel Mbogo |
| 3. | Usaliti Mjini | Francis Imbuga |

C.USHAIRI

| NA. | JINA LA KITABU | JINA LA MTUNZI |
|---|---|---|
| 1. | Fumbo linaloelea | Nyambari C.M.Nyangwine |
| 2. | Malenga wa Ziwa kuu | Wallah Bin Wallah |
| 3. | Andamo,Msafiri Safarini | Mohammed Khelef Ghassani |
| 4. | Wosia wa Baba. | Ahmed Mohamed Amanzy |

2. ORODHA YA VITABU TEULE KIDATO CHA TANO NA SITA MTAALA MPYA:FASIHI YA KISWAHILI

A:RIWAYA

| NA. | JINA LA KITABU | JINA LA MTUNZI |
|---|---|---|
| 1. | Vuta N'kuvute | Shafi Adam Shafi |
| 2. | Asali chungu | Said Ahmed Mohamed |
| 3. | Mwana wa Yungi Hulewa | Mohammed Said Abdulla |
| 4. | Vipuli vya Figo | Emmanuel Mbogo |

B.TAMTHILIYA

| NA. | JINA LA KITABU | JINA LA MTUNZI |
|---|---|---|
| 1. | Kaputula la Marx | Euphrace Kezilahabi |
| 2. | Nyerere na Safari ya Kanaan | Emmanuel Mbogo |
| 3. | Morani | Emmanuel Mbogo |

C.USHAIRI

| NA. | JINA LA KITABU | JINA LA MTUNZI |
|---|---|---|
| 1. | Dhifa | Euphrace Kezilahabi |
| 2. | Utenzi Majumui wa Karne ya 21 | Idd M.Mwimbe |
| 3. | Malenga wa Bara | M.M.Mulokozi & K.K.Kahigi |
| 4. | Fungate ya Uhuru | Mohamed Seif Khatibu |